



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA NISHATI

MAMLAKA YA UDHIBITI WA
HUDUMA ZA NISHATI NA MAJI
(EWURA)



TAARIFA KWA UMMA

(Imetolewa chini ya Kifungu na 19(2) (a) cha Sheria ya EWURA, Sura ya 414)

TAARIFA inatolewa kwa umma kuwa Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) imepokea maombi ya leseni kutoka kwa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Babati (Babati WSSA) (“Muombaji”) kwa ajili ya kutoa huduma za majisafi na usafi wa mazingira katika eneo la Babati mjini na Miji ya Bashnet, Dareda, Gallapo, Magugu na Katesh; zilizopo Mkoa wa Manyara. EWURA inakaribisha maoni kutoka kwa wananchi juu ya maombi hayo. Maelezo ya Muombaji ni kama yalivyotolewa hapa chini:-

1: Jina na Anuani:

Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Babati,
S.L.P 245,
Babati.
Tanzania.
Barua Pepe: info@bawasa.or.tz

2: Maelezo ya Leseni:

Leseni ya kutoa huduma za Majisafi na Usafi wa Mazingira katika eneo la Babati Mjini na Miji ya Bashnet, Dareda, Gallapo, Magugu na Katesh.

3: Chanzo cha Maji na Miundombinu

Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Babati ina vyanzo vikuu viwili vya maji ambavyo ni maji ya chini ya ardhi na maji ya juu ya ardhi. Vyanzo vya chini ya ardhi vinajumuisha visima virefu ishirini na tatu (23) na vyanzo vya juu ya ardhi vinajumuisha vyanzo kumi na mbili (12) vya chemchem na mto. Jumla ya uwezo wa kuzalisha maji kwa vyanzo vyote ni mita za ujazo 29,240 kwa siku. Miundombinu ya uzalishaji na uhifadhi maji ya muombaji inajumuisha; matenki ya maji sitini na moja (61) yenye uwezo wa kuhifadhi maji kiasi cha mita za ujazo 5,454. Muombaji pia

ana mtandao wa majisafi wenye urefu wa kilomita 758.11km pamoja na vilula 283.

4: Umiliki

Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Babati inamilikiwa kwa asilimia 100 na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mtu yeyote mwenye maoni au pingamizi kuhusiana dhidi ya maombi tajwa hapo juu, awasilishe kwa maandishi EWURA kwa anwani iliyotajwa hapa chini ndani ya siku ishirini na moja (21) kuanzia siku ya kuchapishwa kwa tangazo hili. Nyaraka za maombi ya leseni zinaweza kuoneshwa kwa mtu yeyote kwa maombi maalum ya maandishi.

Kaimu Mkurugenzi Mkuu

Mamlaka ya Udhhibiti wa Huduma za Nishati na Maji
Jengo la EWURA, Kiwanja Na 3, Kitalu AD, Medeli Magharibi
S. L. P 2857, Dodoma.

Simu: +255-26 2329003-3; Nukushi: +255-26 2329005;

Namba ya Bure 0800110030;

Barua pepe: info@ewura.go.tz

Tovuti: <http://www.ewura.go.tz>